Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.41 - 2025*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

# Sasa Rasmi




# Rais Samia asisitiza utekelezaji wa Sera na Mitaala iliyoboreshwa

**- KAZI IENDELEE -**





## BODI YA UHARIRI

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia


# TAHARIRI

## Sera mpya ya Elimu nyenzo muhimu maarifa na ujuzi

Februari Mosi Mwaka 2025, Tanzania ilishuhudia tukio la Kihistoria la Uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023. Uzinduzi wa tukio hilo muhimu ulifanywa na Mhe. Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, unatajwa kuwa hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa Taifa linapata maendeleo endelevu kupitia elimu bora na mafunzo.

Ikumbukwe kuwa Sera hii inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye ya Taifa. Aidha itasaidia itasaidia kutoa mwongozo wa jinsi ya kuboresha elimu na mafunzo, kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu kwa wote, na kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali za elimu.


Moja ya malengo makuu ya Sera hii ni kuhakikisha kuwa elimu inapatikana kwa wote bila ubaguzi wowote. Hii inajumuisha kutoa fursa sawa kwa watoto wa kike na wa kiume, watu wenye ulemavu, na makundi mengine maalum. Kwa kufanya hivyo, Tanzania inatarajia kuongeza kiwango cha ushiriki wa wanafunzi katika elimu na kupunguza idadi ya watoto wanaoacha shule.

Aidha, sera hii inasisitiza umuhimu wa kutumia teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwezesha wahitimu kupata maarifa, stadi na ujuzi stahiki unaohitajika katika karne ya 21 ambao utaimarisha umahiri katika ushindani wa soko la kimataifa.

Kwa upande wa mafunzo, Sera hii inalenga kuboresha mfumo wa mafunzo ya ufundi na stadi za kazi ili kuhakikisha kuwa vijana wanapata ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Hii itasaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana na kuongeza tija katika sekta mbalimbali za uchumi.

Pia, Sera inasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika kutoa mafunzo na fursa za ajira kwa vijana.





## Sera Mpya ya Elimu >



# Rais Samia asisitiza utekelezaji wa Sera na Mitaala iliyoboreshwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kuwezesha na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Mitaala mipya ya Elimu, ili ilete matokeo yaliyokusudiwa katika kuimarisha sekta ya elimu.

Rais Dkt. Samia ametoa agizo hilo Februari Mosi, 2025 jijini Dodoma akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la Mwaka 2023.




Rais Dkt. Samia amesema mabadiliko na kukua kwa kasi kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kunaweza kuwa na mchango chanya au hasi kutokana na namna jamii itakavyojipanga, hivyo ili kuendana na mabadiliko hayo ni lazima kutumia TEHAMA kutoa elimu kwa urahisi na kuwandaa vijana wetu kuwa na taaluma na ujuzi wa taaluma zinazoenda na mageuzi ya TEHAMA bila kuathiri maadili ya vijana hao.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amesema Serikali haina budi kuwa na maandalizi ya kutosha kwa kuinua viwango vya ubora wa elimu, na kuwandaa vijana vizuri zaidi ili waweze kumudu stadi muhimu zitakazowawezesha kuajiriwa na kujiajiri pamoja na kuwajengea ujasiri na kuweza kujiamini.

Rais Dkt. Samia pia amesema dhamira ya kufanya mabadiliko katika Sera ni kumuandaa kijana anayejiamini na mwenye nyenzo stahiki za kukabiliana na ushindani wa kikanda na kimataifa ili, kwa kutumia utajiri wa rasilimali zetu, aweze kunufaika kiuchumi.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa kupitia Sera ya Elimu iliyoboreshwa, mwanafunzi amalizapo shule ya sekondari, atakuwa na ujuzi na stadi zitakazomuwezesha kutoa mchango kiuchumi kwa jamii inayomzunguka na taifa kwa ujumla.

Sera iliyoboreshwa pia italeta somo la ujasiriamali ambalo litakuwa la lazima kwa kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne kwa lengo la kumuandaa mwanafunzi kupata misingi ya biashara, ili akiamua kujiajiri kwa kutumia stadi alizopata shuleni, aweze kufanya shughuli zake akiwa na maarifa ya biashara na apate manufaa zaidi.

Vilevile, ili kumuandaa kijana kushindana kikanda na kimataifa, wanafunzi watajifunza lugha mbalimbali za kimataifa ikiwemo kichina, kifaransa na kiarabu ambazo zitawapa umahiri wa lugha, watapata nyenzo muhimu ya mawasiliano na kuwawezesha kufanya biashara kikanda na kimataifa bila kikwazo cha lugha na zitawafungulia fursa mbalimbali zitokanazo na utandawazi.

Rais Dkt. Samia amesema Serikali itapitia upya maslahi ya kada ya walimu nchini ili kuipa hadhi inayostahiki kwa kuwa kada hiyo ndio msingi wa taaluma zote, pamoja na kuendelea kuajiri walimu wenye sifa na kuwapa mafunzo stahiki ili waendane na mwelekeo wa Sera mpya.

Sera Mpya ya Elimu >

# Sera Mpya ya Elimu itawezesha Elimu na Ujuzi - Dkt. Mpango



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema Sera mpya ya Elimu itasaidia kubadili mfumo wa elimu Nchini ili kuwezesha Taifa kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi wa kumudu mabadiliko ya teknolojia kama vile akili mnemba pamoja na ushindani mkali wa kibishara duniani.

Mhe. Mpango amesema hayo Februari 01, 2025 jijini Dodoma akizungumza katika Uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 ambapo amesema kuwa ili kuyakabili mabadiliko ya teknolojia yanayoenda kwa kasi hivi sasa, Sera mpya ya elimu inapaswa kuakisi kikamilifu mabadiliko hayo.

"Sera ya elimu kimsingi ni kanuni ambazo ndizo zinatuongoza tuweze kufikia maamuzi kuhusu maendeleo ya elimu na kufikia malengo yetu kama Taifa. Sera ndio mwongozo wa kuandaa mtaala wa elimu ambao ndio mpangilio wa mambo ambayo Mwanafunzi anatarajia kusaidiwa kujua hatua kwa hatua" alisema Mhe. Mpango.

Dkt. Mpango amesisitiza kuwa Duniani kote, elimu ndio chombo muhimu katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, nyenzo ya kuongeza maarifa na ujuzi, kujenga uwezo wa kufikiri na kuchambua mambo kwa umakini pamoja na kujenga maadili mema na utaifa.

Makamu wa Rais ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kikamilifu mchakato wa mapitio ya Sera hiyo na maboresho ya Mitaala.

Sera Mpya ya Elimu >

# 'Mabadiliko ya Sera ya Elimu yametokana na maono ya Rais Samia'




Chimbuko la mabadiliko makubwa na ya kihistoria katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 yametokana na maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeagiza kufanya mapitio ya Sera hiyo, ili kuendana na mahitaji ya Taifa yanayodhamiria kupata wahitimu wenye Maarifa, Stadi na ujuzi.

Akizungumza katika hafla ya Uzinduzi wa Sera Mpya ya Elimu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema, Wizara ilitekeleza kwa ufanisi mchakato wa mapitio ya Sera ya Elimu kwa kushirikisha wataalam na makundi mbalimbali ya wadau.

"Maua tunayopewa katika hatua hii tuliyofikia tunayapokea, lakini chimbuko la mambo haya ni maono yako Rais Dkt. Samia, hivyo nakupongeza sana kwa dhamira ya dhati iliyotufikisha hapa tulipo" alisema Waziri Mkenda.

Waziri Mkenda amesema elimu itakuwa ya lazima kutoka miaka saba na kuwa 10 na kwamba ilitokana na wanafunzi kumaliza elimu ya msingi wakiwa na umri wa miaka 13 na hivyo kukosa sifa ya kuajiriwa na kujiajiri huku hawana elimu ya ufundi na kwa sasa kupitia sera hiyo itamuwezesha kijana kuingia kwenye uzalishaji.

Waziri huyo amemuahidi Rais Dkt. Samia kuwa Wizara hiyo itasimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera mpya ya elimu ili kufikia azma ya Serikali ya kuzalisha wahitimu mahiri wenye maarifa, stadi na ujuzi stahiki.



Sera Mpya ya Elimu >

# Kikwete: Kongole Serikali kuzindua Sera Mpya ya Elimu

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Ushirika wa Kimataifa wa Kusaidia Maendeleo ya Elimu Duniani (GPE) na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amesema kuwa tukio la uzinduzi wa Sera ya Elimu linaashiria kilele cha mchakato mzima uliofanywa na Serikali katika kuhakikisha sekta ya elimu inaendelea kukua na kuendeleza mahitaji muhimu kufikia viwango vya juu vinavyokidhi mahitaji ya Taifa na Kimataifa.



Mhe. Kikwete ameeleza hayo Februari 01, 2025 jijini Dodoma akizungumza katika halfa ya uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, ambapo ameipongeza Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanya uwekezaji mkubwa ikiwemo ujenzi wa miundombinu ngazi mbalimbali za elimu pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

''Sisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tumepewa fedha Shilingi Bilioni 49, miradi hii mikubwa si kwamba inasogeza karibu huduma ya elimu, bali inasaidia kuboresha mazingira ya kujifunza na kujifunzia alisema Mhe. Kikwete.



Mhe. Kikwete amempongeze Rais Dkt. Samia kwa kuwa na mahusiano na ushirikiano mzuri na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo GPE. Ameongeza kuwa Wadau mbalimbali wa Maendeleo wanafuatilia kwa karibu hatua mbalimbali za Maendeleo na kwamba wanaridhishwa na mageuzi makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu.

Mageuzi Makubwa Sekta ya Elimu >




# Tumeshuhudia Serikali imefanya mageuzi makubwa Sekta ya Elimu

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson ameipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya katika kuhakikisha Taifa linapata elimu bora, ambayo itasaidia kupiga hatua katika Nyanja mbalimbali za kimaendeleo.



Mhe. Ackson ametoa pongezi hizo katika hafla ya Uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, ambapo amesema uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewezesha mageuzi makubwa ya elimu katika ngazi mbalimbali.

"Tumeshuhudia mabadiliko makubwa sana katika sekta hii ya elimu. Bunge ni moja wa wadau ambao wameshirikishwa kikamilifu katika Sera hii, tulipata nafasi ya kutoa maoni, hivyo tunaamini maoni yetu yamejumuishwa na mengine mtaendelea kuyafanyika kazi" alisema Mhe. Ackson.

Kiongozi huyo ametahadharisha kuwa ni muhimu kuangazia mabadiliko ya yanayotokea ulimwenguni yanayochagizwa na teknolojia, ili utoaji wa elimu uende sambamba na mabadiliko hayo.

Ni fursa nzuri kuanza kwa kila mmoja wetu aliyeshiriki katika uzinduzi wa Sera mpya ya Elimu kuangalia namna utakavyoshiriki katika utekelezaji wa Sera hii, ukiangalia matumizi ya teknolojia huko nyuma sisi tulikaririshwa kichwa, ni muhimu kuzingatia mabadiliko kuenda na Sera mpya.

Na sisi kama Bunge tutakuwa tayari kushauri na kubadili sheria ili kwenda sambamba kuwezesha kufikia malengo ya Taifa.

Maendeleo ya Elimu >

# Wadau wa maendeleo wapongeza ushirikiano chanya na Serikali ya Tanzania

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia Dkt. Huma Kidwai amesema Benki hiyo inajivunia mashirikiano chanya na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali ya sekta ya elimu.

Ameeleza hayo Februari 01, 2025 jijini Dodoma akizungumza katika uzinduzi wa Sera mpya ya elimu, ambapo amesema kuwa kupitia miradi mbalimbali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Benki hiyo imetoa ufadhili wa Dola za Marekani Bilioni 1.5 kupitia Mradi wa kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi (BOOST), Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Dkt. Huma Kidwai ametaja miradi mingine kuwa ni Mradi wa Ujuzi wa Mabadiliko ya Afrika Mashariki na Ushirikiano wa Kikanda (EASTRIP), Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) na Mradi wa Kuboresha Ubora wa Elimu ya Msingi Zanzibar (ZIQUE).

"Sasa tupo katika maandalizi ya Mradi mpya wa awamu ya pili wa Elimu na Ujuzi kwa Ajira Zenye Tija (ESPJ II)" Alisema Mkurugenzi huyo.

Naye Mwenyekiti Mwenza wa Wadau wa Maendeleo kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) Zulqarnain Hussain Anjum amesema Wadau hao wanazitambua kwa dhati juhudi mbalimbali za Serikali katika kutekeleza mageuzi makubwa ya elimu yanayolenga kujenga maarifa na ujuzi stahiki kwa watanzania ili kuchochea maendeleo.







# Picha: Uzinduzi Sera Mpya ya Elimu >




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaini bango maalum lenye ujumbe kuhusu elimu, baada ya kukagua mabanda ya maonesho ya masula ya elimu katika viwanja vya ukumbi wa Mikutano wa Jakaya KJkwete Jijini Dodoma Februari Mosi 2025.***




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo maalum kutokana na maono na mchango wake kwenye sekta ya elimu kutoka kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda***

# Picha: Uzinduzi Sera Mpya ya Elimu >



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi cheti maalum cha pongezi Mwenyekiti wa Kamati ya Mapitio ya Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo, Profesa Joseph Semboja katika hafla ya uzinduzi wa Sera hiyo Februari Mosi, 2025, jijini Dodoma.*



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi cheti maalum cha pongezi Mwenyekiti wa Kamati ya kuandaa Mitaala ya elimu Profesa Makenya Maboko katika hafla ya uzinduzi wa Sera hiyo Februari Mosi, 2025, jijini Dodoma.*

# Picha: Uzinduzi Sera Mpya ya Elimu >




***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akikagua maonesho katika uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo kwa mwaka 2014, toleo la 2023, uliofanyika Februari Mosi 2025 Jijini Dodoma.***



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz